SERIKALI YA KAUNTI YA TURKANA

AFISI YA GAVANA

HOTUBA YA MHESHIMIWA JOSPHAT KOLI NANOK, GAVANA WA KAUNTI YA TURKANA WAKATI WA SHEREHE ZA SIKU KUU YA MASHUJAA YA MWAKA WA TISA, OKTOBA 20 2018, KATIKA BUSTANI ZA MOI, LODWAR.

Naibu wa Gavana, Kaunti ya Turkana,
Mheshimiwa Seneta,
Spika wa Bunge la Turkana,
Mshirikishi wa Serikali ya Kitaifa katika Kaunti,
Wabunge wa Kitaifa,
Wabunge wa Kaunti,
Maafisa wa Serikali ya Kaunti na ile ya Kitaifa,
Wakaazi huru wa kaunti ya Turakana.

Wakenya Wenzangu,

Leo ni heshima kuu kwangu kujiunga nanyi na wakenya wengine nchini kuadhimisha sherehe za siku kuu ya mwaka wa tisa ya Mashujaa; siku ya kuwaheshimu mashujaa wetu waliochangia katika ujenzi wa taifa hili tukufu.

Tumekusanyika hapa kukumbuka kujitoa mhanga kwa wake na wanaume; kutoka kudhihirisha uzalendo kwa kupigania uhuru kulikomboa taifa hili kutoka minyororo ya wakoloni na kuitisha utawala, hadi kwa wazalendo walioongoza harakati za kuleta demokrasia miaka ya tisini ambayo ilileta mabadiliko ya kisiasa na kusababisha kuidhinishwa kwa Katiba mpya mwezi Agosti mwaka wa 2010.

Kwetu sisi na mashujaa hao, sherehe za kuadhimisha siku kuu ya Mashujaa, ni jukumu letu la kitaifa. Ni desturi ambayo twapaswa kuwakabidhi vizazi hadi vizazi, kwamba kamwe Wakenya hawapaswi kusahau kuwa katika kipindi kigumu cha histroria ya taifa letu, waume kwa wake wajasiri walisimama kidete walipohitajika kuonyeha msimamo wao.

Hebu maisha ya Mashujaa hawa yaendelee kuwapa motisha kizazi cha sasa na vizazi vijavyo kama ukumbusho kuwa sote tunawajibikia nchi hii kwa kuzingatia na kutetea haki na uhuru ulioko katika katiba na kuendelea kukabiliana na umaskini, maradhi na kutojua kusoma na kuandika mbali na kuimarisha maisha ya raia wenzetu.

Mabibi na Mabwana,

Hebu nitambue kundi la mashujaa waliojitoa mhanga kukomesha mzozo baina ya jamii za Ateker zinazoishi katika mpaka wetu na Uganda na Sudan Kusini ambako wengi walipoteza maisha yao katika hali ya kung’ang’ania raslimali; na kuleta enzi mpya ya kuishi pamoja kwa amani ambayo imedumu kwa miaka 45 na ambayo sasa tumeanza kufurahia matunda yake kikamilifu.

Mashujaa hawa ni Mzee Tioko Looyakasiwan, David Olocho – ambaye alikuwa Mkuu wa Wilaya ya Turkana mwaka wa 1973, aliyekuwa Mwenyekiti wa Baraza la Wilaya ya Turkana - Kuya Ekomwa, Aliyekuwa Jenerali wa Nging'oroko Losike Engor, aliyekuwa paramount chief wa Loima, Imana Ebei, –Mzee Idere Limangole na aliyekuwa chifu wa Lokiriama, Ekuleu Boyel. Daima majina yao yatasalia katika mnara wa amani wa Lokiriama na katika mioyo ya vizazi ambavyo vitafurahia ustawi wa kijamii na kiuchumi unaotokana na amani hii. Amani katika ushoroba huu itatumika kama kigezo cha kuendelea kututia moyo katika juhudi za kukomesha mizozo katika mipaka yetu mbali mbali na ni ushahidi kwamba wakati jamii zinajitolea kuimarisha amani, na kwa mchango wa serikali na washika dau wote wa Amani, bila shaka tutaweza kuafikia kikomo cha mzozo.

Wakenya wenzangu,

Tukiwa kaunti, tunajiunga na Wakenya wenzetu kusherehekea ufanisi tulioafikia kisiasa na kiuchumi. Sisi tumenufaika na matunda ya katiba mpya ambayo ilituletea ugatuzi na raslimali ambazo tumewekeza katika kipindi cha miaka sita kustawisha Turkana na kuimarisha riziki za watu wetu.

Siku hii pia inatupa fursa kutafakari ufanisi wa maendeleo tuliyoyapata tukiwa Kaunti katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita wa matumizi ya pesa za serikali, na hatua tulizochukua katika kutimiza malengo yetu ya maendeleo chini ya jukumu tulilopewa na wakaazi wa Turkana.

Utekelezaji wa malengo yetu ya maendeleo katika miaka michache iliyopita umekuwa ukivurugwa na tatizo la mara kwa mara la kucheleweshwa kwa fedha na hazina ya kitaifa. Hali hii imeathiri shughuli za kaunti ikiwemo malipo ya gharama za shughuli na maendeleo.

Kupitia Baraza la Magavana, tumewasilisha malalamishi yetu kwa Serikali ya Kitaifa kuhusu kucheleweshwa kwa pesa na tunatumai hali hii itabadilika hivi karibuni.

Vile vile, tumeelezea kutoridhika kwetu na jinsi hazina ya kitaifa inavyofanya maamuzi kiholelaholela kupunguza fedha zilizotengewa kaunti bila mashauriano kati ya serikali za kaunti na ile ya kitaifa.

Tunajua hatua hii ya kupunguza fedha kwenye kaunti zitaathiri pakubwa bajeti za serikali za Kaunti. Kaunti ya Turkana itakuwa na upungufu wa shilingi milioni 310, hali ambayo itaathiri utoaji huduma na hivyo kuchelewesha utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Nina furaha kutangaza kwamba Mpango wa Pili wa Ushirikishi wa Maendeleo ya Kaunti tayari umeidhinishwa na Bunge la Kaunti ya Turkana baada ya utaratibu na ushirikishi wa mikutano ya umma iliyofanywa na serikali na bunge la kaunti kwa ushirikiano na washirika wetu wa kimaendeleo.

Mpango huo mpya utatoa mwongozo kwa serikali za Kaunti, ya kitaifa na washirika wa kimaendeleo ya jinsi ya kuwa na mwelekeo wa pamoja na kujumuisha raslimali zao katika utekelezaji wa ajenda ya maendeleo ya Kaunti ya Turkana.

Kuidhinishwa kwa mpango huo unatoa fursa ya kutumwa kwa fedha na hazina ya kitaifa kwani mpango huu wa ushirikishi wa maendeleo ulikuwa mojawapo wa masharti na msimamizi wa bajeti, ndiposa pesa za maendeleo ziweze kutumwa.

Mabibi na Mabwana,

Wakati wa sherehe za mwaka huu za siku kuu ya Madaraka, niliangazia sehemu tano za mageuzi katika maendeleo tutakazozipa kipau mbele katika kipindi changu cha pili.

Mpango huu wa ajenda tano unazingatia zaidi shughuli za Ustawi wa Maji, Uchimbaji Madini na usimamizi wa Mali Asili, Kujitoshelesha kwa Chakula, Ushirikiano na Uekezaji; Ushirikishi na Matumizi ya Raslimali pamoja na harakati za kuleta amani na upatanishi katika mipaka.

Tumeleta uwiano katika bajeti yetu ya Kaunti ili kuafikia malengo haya matano ya maendeleo.

Kulingana na hali hii, mabibi na mabwana, nataka kuangazia hatua zilizoafikiwa na Serikali ya Kaunti katika kutimiza malengo haya;

Mabibi na Mabwana,

Katika jitihada zetu za kutatua matatizo ya maji ambayo yanaendelea kukumba watu wetu, Seriali yangu inawasiliana na washirika wa kimaendeleo ili kuekeza katika miradi mikubwa-mikubwa ya maji ikiwemo ujenzi wa mabwawa makubwa kote katika kaunti.

Mpango wetu wa kujenga bwawa katika mto wa Tarach, wadi wa Letea katika kaunti ndogo ya Turkana Magharibi unaendelea. Ripoti ya ukaguzi, usoroveya na uchunguzi wa mradi huo ambayo ilitayarishwa kwa pmaoja na Chama cha Msalaba Mwekundu na kufadhiliwa na Shirika la kushughulikia wakimbizi la Umoja wa Mataifa (UNHCR) tayari imekamilika. Kulingana na Mfumo Kamilifu wa Kushughulikia Wakimbizi, mradi huu unakusudiwa kuwashirikisha wakimbizi na wenyeji.

Mradi huu utawanufaisha wakaazi moja kwa moja kupitia kupata maji ya matumizi nyumbani, kunywesha mifugo na uzalishaji wa chakula huko Kalobeyei, Kakuma na viunga vyake.

Hivi karibuni Serikali ya Kaunti itafadhili mkutano wa ana kwa ana na washirika na washika dau kujadili ufadhili wa mradi huu maalumu.

Tukishirikiana na Wakfu wa Hazina ya Kitaifa ya Maji, tunatekeleza miradi ya maji, kuunga mkono ushirikishi wa wakimbizi na wakaazi wa eneo la Turkana Magharibi chini ya ruzuku kutoka kwa Serikali ya Denmark.

Kupitia mgao wetu wa hazina ya usawa na tukishirikiana na halmashauri ya Huduma za maji ya Bonde la Ufa, tunatekeleza miradi ya maji mjini Lodwar ambayo itanufaisha Kanamkemer, St. Mary's na Monti; huku mradi wa maji wa Eliye-Kalokol ukiwa umetekelezwa kwa kiwango kikubwa.

Serikali ya Kaunti imeimarisha kitengo chake cha uchimbaji maji ili kupunguza gharama na hatimaye kuacha kutoa kandarasi za uchimbaji visima vya maji. Katika kipindi kilichopita cha matumizi ya pesa za serikali, tulichimba visima kumi vya maji kwa kutumia vifaa vya kaunti vya shughuli hiyo kwa gharama ya shilingi milioni 22 katika sehemu ambazo zinakumbwa na uhaba mkubwa wa maji.

Mipango inafanywa ili mara tu fedha zitakapotolewa kununuliwe mabomba ya kusukuma maji kwa kutumia vifaa vya kutoa nguvu za umeme kutoka kwa miali ya jua ili kuimarisha kupatikana kwa huduma za maji.

Tukishirikiana na Shirika la GIZ, Serikali yangu imefaulu kuchimba visima 31 vya maji kwa gharama ya shilingi milioni 68 na kuwanufaisha zaidi ya watu 30000 na vituo vya mifugo 62000, ambao sasa hawana matatizo ya kupata maji safi.

Serikali yangu inakusudia kuweka mabomba ya kusukuma maji kwa kutumia nguvu za umeme zinazotokana na miali ya jua katika visima 18 vilivyochimbwa katika kipindi kilichopita cha matumizi ya fedha za serikali. Ukadiriaji umefanywa na zabuni kutolewa za kununua mabomba ya kusukuma maji.

Katika kipindi cha sasa cha matumizi ya pesa za serikali cha (2018/2019), kisima kimoja kimechimbwa kwa gharama ya shilingi milioni mbili katika sehemu ya Nangolekuruk ili kuanza kutumika badala ya kile kilichoko wadi ya Kerio, huku watu 3500 na vituo vya mifugo 5700 wakianza kunufaika na huduma hiyo. Kisima hicho kitawekwa mabomba ya kusukuma maji na tayari vifaa hivyo vimeagizwa kutoka kwa kampuni ya Davies & Shirtliff.

Ili kushughulikia uhaba wa maji na kuimarisha utoaji huduma hiyo, kama njia ya kuhifadhi maji kwa ajili ya jamii za wafugaji.Katika kipindi kilichopita cha matumizi ya pesa za serikali, serikali yangu ilizindua mipango kujenga mabwawa matatu kubwa huko Kotome katika kaunti ndogo ya Kibish, Kalemngorok, Turkana Kusini na Lomelo huko Turkana Mashariki. Uchunguzi, usoroveya na uchunguzi mwafaka kuhusiana na mradi huo utatamatishwa katika kipindi cha sasa cha matumizi ya pesa za Serikali.

Wizara husika pia imeanzisha mfumo wa taratibu 12 za kusambaza maji, huku saba kati yao ikiwa imefanywa kwa ushirikiano na washirika wa kimaendeleo katika sehemu za Lorengelup, Songot, Napeikar, Kalemnyang, Kotela, Lorugum, Kaputir na Nawountos huku huduma hizo zikiwa zimewanufaisha watu 12000 na vituo 28 vya mifugo.

Serikali yangu imeimarisha mfumo wa taratibu tano za kusambaza maji katika sehemu ya Lokori, Kalokol, Kakuma, Lokichar na Lorugum kwa gharama ya

shilingi milioni 100, huku miradi hiyo ikiwa katika viwango mbali mbali.- Tumeanzisha taratibu nyingine nne kwa ushirikiano na shirika la UNICEF na Shirika la Kutoa Misaada la dini ya Katoliki (CRS) lililoko huko Naipa, Kapua na Nakamane.

Idara ya Madini ikishirikiana na Taasisi ya Serikali inayohusika na Mali Asili, imetoa mafunzo kwa maafisa wa kaunti, mashirika ya kijamii, wafanyibiashara na wataalamu kuhusu kiwango cha madini yaliyoko katika kaunti hii.

Mafunzo haya yanasaidia kuwapa shime na kutoa mwongozo kwa washikadau katika sekta ya madini kuhusiana na maongozi ya ustawi wa mali hiyo.

Ni vyema kutambua kwamba, Shirika la Misaada ya maendeleo la Marekani AHADI-USAID, Maongozi na Mswaada wa Kuchimba Madini unaendelea ku-ungwa mkono.

Mapendekezo ya Mswaada huo pamoja na Maongozi yatawasilishwa kwa Baraza la Mawaziri wa Kaunti, wabunge wa kaunti na wananchi ili kuruhusu ushirikishi wa umma kwa wakati ufaao.

Ili kuongeza ushirikishi wa wanawake kupata nafasi katika sekta hiyo ya madini, Idara ya Madini ikishirikiana na Shirika la Wanawake katika sekta hiyo nchini, iliandaa warsha mjini Lodwar ya kuwapasha habari wahusika katika sekta hiyo. Wanawake kutoka kaunti ndogo mbali mbali walinufaika na warsha hiyo.

Hebu nizungumzie jukumu linalotekelezwa na Serikali ya Kaunti na viongozi waliochaguliwa wa Turkana katika kupigania mgao wetu wa mapato katika Mswaada wa Mafuta ya Petroli. Mswaada huu sasa umewasilishwa katika bunge la Seneti ili kuharakisha kupitishwa kwake. Ningependa kuwahakikishia wakaazi

wetu kwamba mjadala mkali kuhusiana na usimamizi wa asilimia tano ya mgao wa jamii utatatuliwa kupitia ushirikishi wa mashauriano na jamii nzima.

Mabibi na Mabwana,

Serikali yangu imetoa kipau mbele kwenye harakati za kujitosheleza kwa chakula, kuimarisha lishe bora na udumishaji wa kilimo, ufugaji na ustawi wa sekta ya uvuvi kama nguzo muhimu ya ajenda ya mageuzi ya Serikali ya Kaunti.

Sekta ya ufugaji ni muhimu sana kwa riziki za maisha ya wakaazi wengi wa Turkana na uekezaji wetu katika sekta hiyo unalenga kuifanya sekta hiyo kuwa ya kibiashara ili kuongeza faida yake.

Mwezi jana nilizindua mpango wa kipekee uliogharimu shilingi milioni 10 wa kuchunguza maradhi ya mifugo kupitia simu za rununu. Mpango huu ulioko chini ya Idara ya Matibabu ya Mifugo, unatoa nafasi ya kushughulikia kwa haraka mkurupuko wa maradhi ya mifugo na hivyo kuunga mkono juhudi za kuzuia kusambaa kwa maradhi hayo. Utaratibu huo umebuniwa kwa msaada kutoka kwa shirika la GIZ na Taasisi ya Kimataifa ya Utafiti wa Mifugo (ILRI).

Tumekuwa tukitekeleza mpango wa dharura wa mifugo na wa kuwanunulia wafugaji mifugo tukishughulikia zaidi maeneo yalioyokumbwa na majanga kama vile ukame, mafuriko na wizi wa mifugo.

Tumezindua mpango huo huko Kasepaeilem, wadi ya Turkwel, kaunti ndogo ya Loima ambako jamii 80 zilipokea mbuzi kumi kila moja huku mpango huo ukisambazwa katika sehemu nyingine za Nakwaperit huko Turkana ya Kati, Lochor-Angierengo katika Turkana Magharibi, Nakinomet katika eneo la Turkana

Kaskazini na Lokamarinyang huko Kibish. Kwa jumla mbuzi 2500 waligawanywa kwa nyumba 347.

Ujenzi wa masoko mapya ya mifugo umekamilika katika miji ya Lodwar na Kakuma na yanasubiri tu kuzinduliwa na kukabidhiwa Chama cha Wauzaji wa Mifugo. Miradi hiyo miwili chini ya mpango wa shirika la USAID unaotambulika kama 'Feed the Future', utazinduliwa karibuni, huku soko la Lodwar likitazamiwa kufunguliwa tarehe 24 mwezi huu wa Oktoba.

Hebu nichukue fursa hii kulishukuru shirika la USAID kwa jukumu lililotekeleza katika kukamilisha miradi hiyo ambayo itachangia pakubwa kwa juhudi zetu za kuifanya sekta ya ufugaji kuwa ya kibiashara.

Serikali yangu imetenga shilingi milioni 40 kwa ujenzi na ununuzi wa vifaa vya maabara ya mifugo mjini Lodwar ambayo itasaidia katika kutambua mapema maradhi ya mifugo. Maabara hiyo itapunguza muda na gharama tunayopata kutuma sampuli kwa Maabara ya Matibabu ya Mifugo ya Kabete jijini Nairobi.

Kuhusu ustawi na uimarishaji lishe ya mifugo, tunapanga kugawa tani 385.4 za chakula cha mifugo ambapo tani 64 tayari zimegawanywa katika kaunti ndogo-ndogo saba za Turkana.

Kazi ya ujenzi wa maghala ya kuhifadhi samaki waliokaushwa unaendelea katika sehemu za Lowareng'ak, Nachukui, Namukuse na Ng'imuriae. Mata tu maghala hayo yatakapofunguliwa, basi yatasaidia katika kupunguza hasara baada ya mavuno.

Vile vile, tumewasaidia wavuvi na vifaa vya kuvua samaki ikiwemo maboya, yavuyavu na makoti ya uokoaji katika wadi za Kerio, Kang'atotha na wadi ya Lakezone.

Mabibi na Mabwana,

Huku kukiwa na uwezo mkubwa katika sekta ya kilimo ambao bado haujatumika kikamilifu, Serikali yangu itatoa raslimali ambazo bado hazitumiki kupanua maeneo ya unyunyizaji maji mashamba, kuleta kilimo cha shughuli mbali mbali ili kuingia katika biashara tofauti-tofauti kama vile utaratibu wa kunyunyiza maji mashamba kwa njia ya pole-pole. Ninasisitiza imani yangu kwamba kaunti yetu inaweza kujitoshelesha kwa chakula na vile vile kuweza kuwa kapu la chakula kwa eneo hili.

Serikali ya kaunti kwa wakati huu inafuatilia kwa makini mkakati wa ufunga-mano na sekta ya kibinafsi katika nyanja za unyunyizaji maji mashamba kwa kil-imo cha kibiashara ili kukuza chakula kingi zaidi kwa ajili ya wakaazi wetu na vile vile kuwa na chakula cha ziada cha kuuzwa katika masoko nje kaunti na kuongezea mapato ya familia.

Kupitia mpango wa Shirika la Chakula Duniani wa Ushirikishi wa kupatikana kwa masoko, mashirika ya wakulima 46 yanayojumuisha wakulima 2600 wamepewa mafunzo kuongezea thamani mazao ya nafaka, kunde na mboga. Zai-di ya wakulima 80000 wamefikiwa na jumbe za wakulima nyanjani kote nchini kupitia ziara za mara kwa mara za makundi na za wakulima binafsi.

Idara ya Kilimo ya kaunti imefanya ukaguzi wa mara kwa mara kuhusiana na magonjwa na wadudu. Zaidi ya familia 3000 zimenufaika na pembejeo, ikiwemo mbegu na vile vile kuongeza uzalishaji .

Kama njia moja ya kuwasaidia wakulima kupitia mpango wa kupatikana kwa masoko, mashirika tisa ya wakulima yaliuza karibu tani 75 za vyakula kwa thamani ya shilingi milioni tatu kwa shule 65 katika muhula wa kwanza wa mwaka huu. Makundi hayo yalitoka Nadapal, Nanye, Kotela, Kabulokor, Napeikar na Kangalita.

Wakulima huko Katilu wameunga mkono harakati za Bamba Chakula za Shirika la Wakimbizi la Umoja wa Mataifa ili kuuza mboga kufikia sasa shilingi 126,000 zimetolewa kwa kambi ya wakimbizi ya Kakuma na katika makaazi ya Kalobeyei.

Wakenya wenzangu,

Harakati za kuleta amani na kuwa na mawasiliano katika mipaka ni sehemu nyingine niliyoipa kipau mbele katika ajenda yangu ya mipango mitano ya kugeuza Kaunti hii, kwani amani, haki za binadamu na uongozi bora ni muhimu katika udumishaji maendeleo.

Katika moyo wa usalama wa kijamii ili kushughulikia changamoto za usalama katika kaunti hii, mwezi Septemba mwaka huu, nilioongoza mikutano miwili na washikadau huko Katilu katika kaunti ndogo ya Turkana Kusini na Lodwa katika Turkana ya Kati.

Kupitia mawasiliano haya kati ya umma , wakuu wa mashirika ya usalama na Serikali ya Kaunti, maazimio yaliafikiwa ya jinsi ya kukabiliana na ukosefu wa usalama wa ndani ikiwemo kuzuka kwa mizozo baina ya jamii, visa vya unajisi, ujambazi na visa vya wizi wa mifugo.

Kama mnavyojua, ukosefu wa usalama umeendelea kuwa changamoto kubwa katika eneo la Turkana Mashariki huku kukiwa na mashambulizi ya mara kwa mara ambayo yamesababisha maafa na wizi wa mifugo. Ninakariri wito wangu kwa vyombo vya usalama wa kitaifa kuimarisha hatua ya kushika doria katika maeneo yanayokumbwa na hali hiyo na kuwasiliana na jamii kuhakikisha usalama unadumishwa ili wakaazi waendelee na shughuli zao za kujitafutia riziki.Ninajua kwamba Inspekta Jenerali wa Polisi, Joseph Boinett amejitolea kuwasil-

iana na jamii na kujadiliana na viongozi wa Kaunti za Turakana na Baringo ili kuleta uwiano na kukomesha misimamo mikali.

Ninaamini kwamba suluhisho la kudumu kuhusiana na ukosefu wa usalama wa mara kwa mara litapatikana kupitia harakati za kuwa na juhudi za pamoja za kuleta amani baina ya kaunti hizi ili kuleta amani ya kudumu katika ushoroba huu unaokumbwa na mizozo. Nayahimiza mashirika ya kijamii yaunge mkono juhudi hizi za serikali.

Serikali yangu imetenga shilingi milioni 60 za kutoa makaazi kwa jamii zilizoathiriwa na mizozo katika kaunti ndogo za Turkana Kusini, Turkana Mashariki na Loima ili jamii hizo zirejee katika ardhi zao za tangu jadi na kurejelea maisha yao ya kawaida na kuendea kujitafutia riziki zao.

Licha ya mchango huu mkubwa wa kuleta amani na usalama, serikali ya kitaifa ndiyo inayowajibikia amani na usalama na hilo jukumu ni la kikatiba kuhakikisha maisha na mali ya wakenya inalindwa.

Huku tukitambua hatari zinazotokana na uchimbaji madini, mabadiliko ya hali ya hewa na miradi ya maendeleo ya haraka ya uchukuzi kama vile mradi wa LAPSSET, serikali yangu na washirika wa kimaendeleo wanawasiliana kuhakikisha mipango inayofaa ya kuwapasha wananchi kuhusu umuhimu wa hatua za kukomesha mizozo na kulinda maslahi ya jamii inatekelezwa.

Ni wiki iliyopita tu ambapo mkutano wa mashauriano kati ya viongozi ulifanyika kuhusiana na ununuzi wa ardhi kwa mradi wa ushoroba wa LAPSSET, huku mkutano huo ukijumuisha Wizara za Ardhi, Mafuta ya Petroli na Madini, Tume ya Kitaifa ya Ardhi na Halmashauri ya Ustawi wa Mradi wa LAPSSET; ambapo nilitoa wito wa kuwa na utaratibu ufaao wa kuwafidia watu na jamii zitaka-

zoathirika kutokana na miradi hiyo ili kuepuka kupingwa kutekelezwa kwa miradi hiyo.
Juhudi za kila mara za serikali yangu kuendelea kuimarisha amani zimesaidia katika kupunguza mizozo.

Kupitia mashauraino kati ya serikali, tumefaulu kuleta utulivu na viongozi wenzetu wa Namorunyang wa jimbo la Namorunyang nchini Sudan Kusini na eneo la Omo nchini Ethiopia.
Hata hivyo, ninafahamu matukio ya hivi majuzi yamevuruga juhudi hizo za kuleta utulivu na kuishi pamoja kwa jamii katika mpaka wa Ethiopia. Serikali yangu inafuatilia suala hilo kwa makini na hivi karibuni itaanza kuwasiliana na wenzetu nchini Ethiopia.
Katika majadiliano ya hivi majuzi na Wizara ya Ugatuzi na inayoshughulikia sehemu kame na zile zisizotumika kikamilifu, nimeona serikali ya Kitaifa imeanza kutilia maanani zaidi juhudi za kuleta amani. Ninafahamu mipango inafikia kilele kati ya Serikali ya Kenya na ya Uganda kuanzisha Mpango wa Amani Mpakani ambao makubaliano yake na utekelezi wa mfumo huo utatiwa saini na Rais Uhuru Kenyatta na Rais Yoweri Museveni kabla ya mwisho wa mwaka huu.

Mpango huu utatoa raslimali zaidi kushirikisha juhudi zote za kuleta amani na kuziweka chini ya mkakati mmoja na kuongeza raslimali za kushughulikia masuala ya huduma za maji, elimu, afya na matatizo ya kibiashara katika mpaka.

Hotuba yangu ya hivi majuzi niliyowasilisha katika Kongamano la kimataifa la wafanya maamuzi na waratibu maongozi mjini New York, kuhusu ufanisi wa harakati za amani zinazoendeshwa na serikali za kaunti, ulizua hamu kwa

wafadhili na washirika wa kimaendeleo kutaka kuunga mkono juhudi za Kenya na Uganda kuleta amani kwa jamii za mpakani.

Ninafahamu kuhusu mikutano ya hivi majuzi kati ya wizara husika za Kenya na Uganda inayokusudiwa kubuni mkakati na mpango wa kushughulikia jamii za mpakani na kuhakikisha ushirikishi unaofaa wa matumizi ya fedha kwa njia nzuri kutoka Mashirika ya IGAD, Muungano wa Ulaya na shirika la UNDP na washirika wengine wa kimaendeleo .

Hatua hii itasaidia kuafikia miradi inayochangia katika amani ya kudumu, ikiwemo ujenzi wa mabwawa makubwa, masoko, vituo vya afya, majosho na shule kwa manufaa ya wafugaji wanaoishi katika mpaka wa Kenya na Uganda.

Mabibi na Mabwana,

Nguzo ya ushirikishi na utumizi wa raslimali inakusudiwa kuziba mapengo yanayotokana na upungufu wa hela zilizotengwa kutokana na mahitaji makubwa ya maendeleo kama yalivyofafanuliwa katika Mpango wa ushirikishi wa Maendeleo ya Kaunti.

Baraza la Maendeleo ya maeneo ya Mpakani katika kaunti inajumuisha kaunti kumi, huku Kaunti ya Turkana ikiwa ni mmoja wa wanachama wa kaunti hizi na Baraza hili limekuwa chombo cha kukusanya raslimali na kushughulikia changamoto za jamii zinazoishi mipakani. Baraza hili linatoa fursa ya kupata ufadhili na matukio ya hivi majuzi yametoa hamu kwa washirika wa kimaendeleo kutoa ufadhili kupitia baraza hili la FCDC.

Tunaendelea na mipango ya kuanzisha utekelezaji wa idara ya ukusanyaji na utumizi wa raslimali, ambazo malengo yake yatakuwa kutafuta fedha na raslimali za ziada ili kupunguza mapengo ya ufadhili.

Mabibi na Mabwana,

Kwa wakati huu, Serikali yangu inachunguza upya Makubaliano tuliyoafikia na washirika mbali mbali wa kimaendeleo. Mikataba hii ni pamoja na ile tuliyoafikiana naTaasisi ya Turkana Basin Institute, Mpango wa Chakula Duniani na Dayosisi ya Lodwar.

Tunaingia awamu mpya mwaka ujao ya Umoja wa Mataifa kuwa na mpango mmoja wa kutoa huduma, kuwa na afisi moja, hazina moja na uongozi mmoja chini ya ushirikishi mmoja.

Mpango huu utaleta uwiano wa mfumo wa Misaada ya maendeleo ya Umoja wa Mataifa ya kipindi cha mwaka wa 2018-2022, Mpango wa ushirikishi wa Maendeleo ya Kaunti wa 2018-2022 na vile vile mpango wa kiwango cha kadri na nguzo nne za ajenda ya Maendeleo ya serikali ya kitaifa ikiwemo mipango ya nyanja tano za kimaendeleo nilizozipa kipau mbele.

Ili kuhakikisha ushirikishi bora wa mipango, utoaji misaada na umiliki wa mpango huu, serikali ya Kaunti ya Turkana na Umoja wa Mataifa zimeanzisha Wakfu wa Hazina ya washirika wa Kimaendeleo. Hazina hii itatumika kushirikisha kwa njia nzuri na kujumuisha raslimali kwa ufadhili wa mipango ya ushirikishi wa maendeleo ya Kaunti. Hazina hii iko wazi kupokea michango kutoka kwa serikali, Umoja wa Mataifa, washirika wa Kimataifa, sekta za Kibinafsi na wahisani.

Shughuli za hazina hii ya washirika wa Kimaendeleo zinaendeshwa kwa njia nzuri. Mfumo wa kisheria umeidhinishwa na hazina ya kitaifa ya serikali ya Kenya na miongozo inakamilishwa na Umoja wa Mataifa na serikali ya Kaunti.

Mabibi na Mabwana,

Ili kuimarisha uwajibikaji wa kifedha, Hazina ya Kaunti imepiga hatua kubwa katika kuweka mifumo ya kifedha inayoendeshwa kwa mitambo na kubuniwa kwa utaratibu wa ununuzi wa bidhaa na utoaji zabuni kwa njia ya mtandao, unaoungwa mkono na Mfumo Unganishi wa Usimamizi wa Kifedha, (IFMIS).

Hivi majuzi, Hazina ya Kaunti ilitoa mafunzo kwa maafisa wakuu wa serikali ya kaunti na kuandaa mpango wa uhamasishaji kuhusu ugavi wa bidhaa wa ku-jiandikisha wenyewe kwa wagawaji bidhaa katika mtandao wa ugavi wa bidhaa wa IFMIS na ununuzi wa bidhaa kwa njia ya mtandao (utoaji zabuni) kwa ushirikiano na hazina ya kitaifa.

Kuhusu ukusanyaji mapato, mikondo yetu ya kujipatia mapato sasa imefikia shilingi milioni 36 kufikia mwisho wa robo ya kwanza ya mwaka, ili hali lengo la mwaka ni shilingi milioni 250.

Katika jitihada za kuimarisha ukusanyaji wa mapato, ununuzi wa mfumo mpya unaonuiwa kuweka mitambo ya kujiendesha yenyewe ya utaratibu wa ununuzi unaendelea. Punde tu mfumo huo utakapowekwa, wafanyi biashara ndogo ndogo watahimizwa kuchukua fursa hiyo ya mfumo usiotumia pesa taslimu kulipia malipo yao.

Mabibi na Mabwana,

Serikali yangu itaendelea kutilia nguvu uhusiano mwema baina ya serikali na kuwekeza ili kuimarisha uhusiano wa kibiashara baina ya mipaka kutokana na kuwepo kwa mapatano ya amani kwenye mpaka. Uhusiano huu mzuri umechangia ongezeko la biashara baina ya mipaka.

Ni wasi sasa kwamba kunao wafanyi biashara 6900 wenye leseni wanaoendesha shughuli zao katika Kaunti ya Turkana kuanzia mwaka wa 2013 hadi sasa, dhi-hirisho tosha hali ya kibiashara imeimarika.

Ili kubuni hali bora ya kufanyia biashara Turkana, mashauriano yanaendelea kujadili kubuniwa kwa ushirikiano wa kibiashara kupitia mikataba ya uelewano, na Halmashauri ya kukabiliana na bidhaa ghushi (Anti-Counterfeit Authority), Taasisi ya mafunzo ya kibiashara nchini(Kenya Institute of Business Training),shirika la Kenya Industrial Estate, na Halmashauri inayosimamia biashara ndogo ndogo na za kadri(Micro and Small Enterprises Authority).

Mabibi na Mabwana,

Ili kupeleka huduma karibu zaidi na wananchi, utawala wangu umejitolea kusambaza zaidi huduma hadi vijijini.

Tumekamilisha uchunguzi wa Mswada wa Utawala wa Vijijini wa mwaka 2018 ambao utawasilishwa upya kwa baraza la mawaziri na baada ya hapo kupelekwa kwa Bunge la Kaunti ili kuidhinishwa.

Mara tu utakapoidhinishwa, sheria itawezesha kuundwa kwa vitengo 156 vya utawala wa vijiji na baraza 780 za vijijini katika wadi zote.

Utoaji kandarasi za kazi na usimamizi kwa kuzingatia utenda kazi utapewa kipau mbele katika utawala wangu. Nina furaha kuripoti kwamba Baraza la Mawaziri ya Kaunti (CECM), Maafisa Wakuu, Wakurugenzi na Manaibu wa Wakurugenzi wametia sahihi mikataba ya utenda kazi. Hii itahakikisha uwajibikaji kwa watu wa Turkana na kuimarisha utoaji huduma.

Isitoshe, Kitengo cha Mikakati ya Utoaji Huduma katika afisi yangu kitatekeleza jukumu muhimu katika kufungamanisha mkakati wa serikali na utekelezaji wa ujumla wa mpango wangu wa utekelezaji wa miaka mitano na kuwezesha kuafikiwa kwa urathi wangu kama ulivyobainishwa kwenye ruwaza yangu ya maendeleo yenye vipengee vitano muhimu katika kipindi changu cha pili.

Mabibi na Mabwana,

Katika mwaka huu wa matumizi ya fedha za serikali, Idara ya Utawala itapeleka maafisa wa utawala 40 katika Chuo cha Kitaifa cha Huduma kwa maafisa wa Polisi huko Meru, ili kuimarisha maarifa na maadili yao kuhusiana na uongozi wa kujitolea kuhudumu pamoja na nidhamu. Hii ni awamu ya pili ya mafunzo haya baada ya ufanisi wa yale yaliyofanywa mwaka wa 2016.

Kutokana na hali ya ukame ambayo huenda ikatokea, serikali yangu iko katika harakati za kununua vyakula ili kusaidia familia zitakazoathirika. Tunatarajia kwamba washirika na wadau watajiunga na juhudi zetu za kuhakikisha wakazi katika maeneo yaliyoathirika hawaathiriwi na ukame huo.

Tumebuni Idara mpya ya Usimamizi wa huduma za Utendaji kazi (Department of Inspectorate Support Services). Utaratibu wa kuajiri Mkurugenzi na Naibu wake unaendelea pamoja na kuzinduliwa kwa muundo wa idara hiyo.

Inatarajiwa kwamba huduma za idara hiyo zitasambazwa hadi kaunti ndogo ili kusaidia kazi za serikali kama vile ukusanyaji wa mapato na kuimarisha utoaji mwingine wa huduma.

Hali kadhalika, tumebuni afisi ya Mkuu wa Sheria wa Kaunti na tumemwapisha Mkuu wa Sheria wa kwanza wa Kaunti ya Turkana Bw. Erastus Ethekon. Hivi karibuni tutaajiri wakili na wanasheria kadhaa wa Kaunti ili kuipa afisi hiyo uwezo na hivyo basi kuweza kushauri Serikali ya Kaunti kuhusu masuala ya kisheria na kuchangia kuhakikisha sheria zinazopitishwa na Bunge la Kaunti zi-naambatana na katiba ya Kenya.

Mabibi na Mabwana,

Serikali yangu imewekeza kiasi kikubwa katika sekta ya Afya kama kipao mbele kupitia kuongeza mipango muhimu na kushirikiana na washika dau wa maendeleo kuhakikisha kupatikana na kutolewa kwa huduma bora za afya kwa wote.

Ufanisi mkubwa umepatikana katika hospitali ya Lodwar County Referral ambao ni pamoja na kitengo kipya cha ajali na huduma za dharura. Kitengo hicho ambacho kilizinduliwa tarehe 9 mwezi Agosti mwaka huu, kina vifaa vyote vinavyohitajika na kinaweza kuhudumia kikamilifu visa vyovyote vya dharura. Kitengo hicho pia kinajumuisha kliniki maalum na chumba cha kufanyia upasuaji.

Pia mnamo mwezi Agosti chumba kipya na chenye vifaa vya upasuaji cha kujifungulia kwa kina mama pamoja na kitengo cha kujifungulia kwa kina mama kilichofanyiwa ukarabati vilizinduliwa katika hospitali ya Lodwar County Referral. Wodi hiyo ya kujifungulia kwa kina mama ni pamoja na nyingine nne huko Lodwar, Lowareng'ak, Kerio na Kang'atotha zilizojengwa kwa usaidizi kutoka kwa shirika la UNICEF. Wodi hizo ni za kiwango cha juu na zitaimarisha pakubwa maarifa ya kujifungulia hospitalini na kupunguza kwa ujumla vifo vya watoto wachanga na kina mama wakati wa kujifungua.

Katika moyo wa kusambaza huduma maalum za afya, vyumba vipya vya upasuaji vimejengwa na viko tayari kuzinduliwa katika hospitali ndogo za Kaunti za Lorugum na Katilu. Hizi zitapunguza idadi ya wagonjwa wanaotumwa katika hospitali ya Lodwar na zinatarajiwa kuhudumia baadhi ya visa vya dharura vya upasuaji katika sehemu za mashambani.

Hospitali ya Lodwar County Referral sasa ina mitambo mitano ya kusafisha figo au dialisisi, ya kwanza ya aina yake katika Kaunti ya Turkana. Kufikia sasa, vi-

pindi saba vya dialisisi bila malipo vimefanywa kwa ufanisi. Mitambo hiyo imepunguza idadi ya wagonjwa waliokuwa wakitumwa nje ya kaunti kwani matatizo ya dialisisi ya figo yalikuwa mojawapo ya sababu tatu zilizofanya wagonjwa kutumwa nje haswa katika hospitali ya Moi Teaching and Referral Eldoret.

Kadhalika tumejenga na kuweka vifaa chumba cha kuhifadhia maiti chenye uwezo wa kuwekwa miili 66, hii imeongezeka kutoka idadi ya hapo awali ya miili 12.

Kitengo chetu cha matibabu ya meno kimefanyiwa ukarabati na kuwekwa vifaa vyenye uwezo wa kutibu matatizo mbalimbali kama yale ya kizizi cha meno, kujaza jino, kusafisha, matatizo ya taya, na upasuaji mdogo wa kinywani badala ya kushughulikia tu ungo'aji wa kawaida wa meno na elimu ya usafi wa kinywani.

Uhusiano mzuri wa kikazi baina yetu na serikali ya kitaifa umewezesha serikali ya kitaifa kujenga jengo huko LCRH ambalo litawekwa mitambo 64 CT scan ya kuchunguza maradhi ambayo itawekwa hivi karibuni. Mitambo 34 ya CT scan ambayo imekuwa ikitumika huko Lodwar itapelekwa katika hospitali ndogo ya kaunti ya Lopiding.

Kuna harakati za upasuaji wa macho zinazoendelea huko Lokitaung na maeneo mengine ya kaunti ndogo ya Turkana Kaskazini.

Shughuli hii imeungwa mkono na madaktari wa macho ya Uhispania na wa humu nchini. Kufikia sasa, takriban upasuaji wa macho 250 umefanywa kote katika kaunti, haswa kutibu ugonjwa wa macho unaofahamika kama mtoto wa jicho (cataracts) miongoni mwa magonjwa mengine ya macho yaliyoenea kwa wingi.

Ni muhimu kutambua kwamba kwa wakati huu kaunti ina hifadhi ya kutosha ya madawa katika vituo vyote vya afya vinavyofanya kazi kama inavyohitajika ili kutoa huduma ya hali ya juu ya afya.

Mabibi na Mabwana,

Sekta ya elimu imesalia kuwa muhimu kwa serikali yangu. Mnamo mwezi Septemba; walimu 15 wa chekechea waliajiriwa na kupelekwa kufanya kazi katika vituo mbalimbali vya chekechea kote katika Kaunti.

Tunapanga kuajiri walimu 300 zaidi wa chekechea kabla ya mwisho wa mwaka wa matumizi ya fedha za serikali mwaka huu.

Hii inanuiwa kuimarisha idadi ya walimu wa chekechea kutoka 275 hadi 575 katika vituo vya kaunti.

Katika mpango wa serikali ya kaunti wa lishe shuleni, tumepeleka vyakula katika vituo 800 kote katika kaunti katika kipindi cha robo ya mwisho ya mwaka huu. Serikali imetia sahihi mkataba wa maelewano na shirika la Mpango wa Chakula Duniani, taasisi ya Mary's Meal kuhusiana na masuala mbalimbali kama uimarishaji wa wafanyakazi na mpango wa lishe shuleni.

Nina furaha kutangaza kwamba kutokana na uwekezaji katika sekta ya elimu ya chekechea, ECDE, idadi ya watoto wanaojiunga na shule imeongezeka kutoka 94718 hadi 105088 katika muda wa miezi mitatu iliyopita.

Vituo vyote vya utoaji mafunzo ya kiufundi katika Kaunti ya Turkana vimeidhinishwa na kusajiliwa kama vituo rasmi.

Utawala wangu umejitolea kuunga mkono vituo vya mafunzo ya kiufundi na ninahimiza Halmashauri ya Utumishi wa Umma ya Kaunti kuharakisha mpango wa kuwapeleka kwenye vituo mbalimbali wakufunzi 22 wa kiufundi ambao waliajiriwa hivi majuzi.

Serikali yangu inatambua usaidizi mkubwa ambao washirika wetu wanatoa kusaidia ajenda yetu ya maendeleo. Hazina ya Lundin imeshirikiana na Taasisi ya Mafunzo ya Kiufundi ya Rift Valley katika masuala ya huduma za ushauri ili kubuni mipango endelevu ya kuendesha shughuli katika kituo cha mafunzo ya kiufundi cha Lodwar. Pamoja na hayo, Hazina ya Lundin ilisaidia kufanyia ukarabati mabweni ya wavulana na wasichana katika kituo cha mafunzo ya kiufundi cha Lodwar na kununua vitanda 60 vya ghorofa.

Kampuni ya Tullow Oil ilijenga ukuta wa kuzingira, ikaweka langoni kuu na nguvu za umeme katika kituo cha mafunzo ya kiufundi cha Lokichar na pia kutoa mtambo wa jenereta na madarasa matano kwa kituo cha kiufundi cha Lodwar.

Kuhusu ugawaji wa msaada wa elimu, mgao wa mwisho wa shilingi milioni 13 ulinufaisha wanafunzi 13412 wanaohitaji msaada. Tunatarajia mgao ujao utakaotolewa mwezi Novemba wa shilingi milioni 172 utanufaisha wanafunzi 15000 masikini.

Tunaendelea kuimarisha na kujihusisha na michezo mbalimbali katika kaunti kwa kuunga mkono wanamichezo kushiriki katika mashindano nje ya Kaunti yetu.

Mbio za kwanza za masafa marefu, Tobong'u Lore marathon, zilifanyika mwaka huu na zitaandaliwa kama sehemu ya Tamasha za Utalii na Kitamaduni.

Wakati wa mbio za marathon za Eldoret City, Samuel Lomoe kutoka Kokuro aliibuka wa saba.

Ningependa kupongeza timu yetu ya kandanda ya wavulana ambayo ilimaliza nafasi ya pili kwenye mashindano ya chama cha vijana kinachohusisha kaunti mbalimbali nchini, Kenya Inter-County Youth Association, yaliyofanyika huko Makueni.

Kaunti ya Turkana ilishiriki katika mbio za Isiolo Desert Wheel ambapo wanariadha wetu walifanya vyema zaidi na kunyakua nafasi ya pili nyuma ya kaunti ya Nairobi. Mashindano hayo yalinuiwa kutetea haki za watu wanaoishi na ulemavu na nina furaha kwamba tuliwakilishwa kikamilifu.

Ili kuunga mkono kuvumbuliwa na kukuzwa kwa vipawa, vifaa vya michezo pamoja na mavazi ya thamani ya shilingi milioni mbili vimegawanywa katika wadi zote katika kipindi cha robo ya mwisho ya mwaka. Ninaamini kwamba kukiwa na usaidizi zaidi uwezo mkubwa wa michezo katika kaunti yetu unaweza kutumiwa kikamilifu.

Ningependa pia kupongeza matokeo bora ya Samuel Lomoe ambaye alishinda mbio za Mexico Marathon na Titus Ekiru mshindi wa mwaka huu wa mbio za China International Marathon zilizofanyika mwezi Agosti.

Mabibi na Mabwana,

Mpango wa Maendeleo Mijini katika Kaunti ya Turkana, Turkana Integrated Spatial Urban Development Plan (ISUDP), unaohusisha vituo vinane vya miji ikiwa ni pamoja na; Lokori, Lokichar, Lorugum, Kalokol, Lowareng'ak, Lokitaung, Lokichoggio na Kakuma uko katika Bunge la kaunti kujadiliwa na kuidhinishwa. Hii inanuiwa kutoa mwongozo wa maendeleo wa vituo hivi vya miji.

Kwa ushirikiano na shirika la UN-Habitat, utawala wangu umeanzisha na kukamilisha matayarisho ya Mpango wa makazi kwa wakimbizi wa Kalobeyei. Dhana hiyo imenuiwa kuwatangamanisha wakimbizi na jamii iliyowapa hifadhi. Mpango huo utawasilishwa kwenye Bunge la Kaunti ili kuidhinishwa.

Serikali yangu inatekeleza Mpango wa Maendeleo ya Maeneo Wazi wa Lodwar kwa ushirikiano na GeoMaps na mpangaji wa shirika la Habitat.

Zoezi hilo linahusisha kugawanya mji huo katika maeneo mbalimbali kulingana na matumizi na kufungua barabara za kupitia na zile ndogo ambazo zimezibwa.

Kuhusu ukusanyaji taka na usimamizi wake, serikali ya kaunti inajitahidi kuufanya mji wa Lodwar na miji mingine kuwa safi kuambatana na Kifungu cha 42 cha katiba. Kutokana na hayo, serikali yangu inenunua lori maalum kusaidia katika ukusanyaji wa taka mjini Lodwar. Barabara pia zimegawanywa na kusimamiwa na maafisa wa kutekeleza sheria kwa usimamizi bora wa takataka.

Ningependa kupongeza Bunge la Kaunti ya Turkana kwa kupitisha ripoti ya kupandisha cheo mji wa Lodwar kuwa manispaa. Hii imetokea wakati unaofaa huku Mpango wa kusaidia miji nchini kupitia kwa shirika la Benki Kuu Duniani ukizindua ruzuku za kusaidia kustawisha miundo msingi mijini kwenye manispaa.

Mojawapo ya miradi ambayo itafadhiliwa na mpango huu ni ujenzi wa mfumo wa kupitisha maji taka ya Lodwar.

Kunao pia wawekezaji wengine wenye nia ya kuwekeza kwenye rasilimali za kawi ya mvuke katika maeneo ya Namakat na Namarunu. Serikali yangu ingali inafanya mashauriano nao kwa lengo la kutia sahihi Mkataba wa Maelewano ili kazi ya ugunduzi na uchunguzi ianze mara moja. Tutahakikisha kwamba katika mashauriano na ushirikiano wowote ule, wananchi wanashirikishwa na kwamba jamii ya sehemu hiyo itakuwa sehemu ya makubaliano yote yanayotiwa sahihi kama ilivyokuwa kwenye mkataba baina ya Serikali ya Kaunti na Kampuni ya Kawi ya Olsuswa huko Katilia Mwezi Aprili.

Kuambatana na ajenda ya Rais ya kuzingatia maeneo manne muhimu ikiwemo utoaji nyumba za gharama nafuu kwa Wakenya, serikali yangu inashirikiana na serikali ya kitaifa kufanikisha mradi huu. Serikali ya Kaunti tayari imetambua ardhi kwa mradi huu katika Chuo Kikuu cha Turkana na Kawalase.

Katika kipindi cha mwaka huu wa matumizi ya fedha za serikali, Idara ya Ardhi na Mipango ya miji itabuni kitengo cha usimamizi wa miji na utekelezaji sheria za udhibiti wa maendeleo huku Lodwar na baadaye kuzipeleka katika maeneo mengine ya miji. Idara hiyo itahakikisha kutekelezwa kwa sheria na kanuni kati-ka mipango ya maeneo ya miji.

Wakenya Wenzangu,

Sekta ya uchukuzi na muundo msingi ni muhimu katika kuwezesha kuafikiwa kwa maendeleo ya kiuchumi na ruwaza ya 2030. Kama Kaunti, tunajivunia kufunguliwa kwa barabara mpya ambazo mbali na kufungua shughuli za biashara pia zitaongeza ukusanyaji mapato kutokana na ongezeko la shughuli za kibiashara. Shughuli ya kurekebisha barabara zilizopo inaendelea na hii itasaidia kukabiliana na visa vya ukosefu wa usalama katika sehemu nyingi za Kaunti kwa kuyafanya maeneo yote kuweza kufikiwa na maafisa wa usalama.

Idara yetu ya uchukuzi inafanya kazi ya viunganisho mipakani na hivi karibuni itatangaza mradi wa urekebishaji barabara iliyoko mpakani ya Letea junction-Lochor Elim-Loreng-Ngamorkirionok-Nakitong'o. Kuajiriwa hivi majuzi kwa maafisa wa kiufundi na kuwepo kwa mashini kutawezesha kuanzishwa kwa barabara ya mpakani ya Lorugum junction-Namoruputh-Lokiriama ambayo ni barabara kielelezo ya Kaunti.

Serikali yangu hivi karibuni itatekeleza mfumo wa usimamizi wa magari wa hali ya juu ulioidhinishwa kimataifa,(ISO certified Fleet Management System), ili kuhakikisha usimamizi bora na ufaao wa magari yote ya serikali ya kaunti. Hatua hii itazuia kutumiwa vibaya kwa magari na kuhakikisha kwamba magari yanatumiwa tu kwa kazi rasmi na kwa wakati ulioidhinishwa.

Mojawapo ya ajenda kuu nne za serikali ya Kitaifa ni nyumba za gharama nafuu. Hatuwezi kuafikia lengo la kuwa na nyumba za gharama nafuu tukipuuza uchukuzi na maendeleo ya muundo msingi.

Idara ya Muundo msingi na uchukuzi inatilia maanani zaidi uchukuzi na maendeleo ya muundo msingi ili kuhimiza uwekezaji wa miradi ya nyumba za gharama nafuu.

Katika kipindi cha sasa cha matumizi ya fedha za serikali, tumeweza kurekebisha viwanda na mitambo yetu ambayo ilikwama na sasa inafanya kazi kusaidia urekebishaji wa barabara katika Kaunti. Wizara ina tingatinga tatu za kutengeneza barabara, tipa tatu, doza mbili, rola moja, tingatinga moja ya kuchimba, moja ya kupakia, moja ya kumwaga maji na moja ya kuhamishia. Serikali yangu iko katika harakati za kununua mashini zaidi kurahisisha kazi ya urekebishaji wa mara kwa mara wa barabara katika kaunti ndogo wakati inapohitajika.

Serikali ya kaunti inaendelea na urekebishaji wa barabara za kaunti ndogo, kwenye mpango uliofadhiliwa na Halmashauri ya Barabara Nchini chini ya Hazina ya Fedha za Urekebishaji Barabara.

Fedha zilizolimbikizwa kutoka kwa miaka miwili iliyopita ya matumizi ya fedha za serikali (FY 2015/2016-2017/2018) zilikuwa shilingi milioni 753.

Kufikia sasa, tumetekeleza miradi 20 inayojumuisha kilomita 1087 na tutatanga za miradi mingine 36 ambayo itajumuisha kilomita 587. Tunapanga kutekeleza awamu ya mwisho ya miradi ya RMLF katika robo ya tatu ya mwaka ambayo itahusisha kuweka changarawe kilomita 15 za barabara katika kaunti ndogo saba huko Turkana.

Zaidi ya hayo, tumeweza kufungua barabara ndogo katika vijiji vitano katika wadi ya Lokichar Turkana Kusini. Tunanuia kuendeleza kazi hii hadi katika kaunti nyingine ndogo ambapo tutasawazisha ardhi na kumwaga changarawe kwenye barabara ndogo katika maeneo ya Napetet, Nakwamekwi, Kanamkemer na Nawoitorong mjini Lodwar.

Utawala wangu pia unaandaa sera ya hazina ya uchukuzi ya Kaunti (CMTF) ambayo itatoa mwongozo wa utekelezaji shughuli za uchukuzi na sekta za magari katika Kaunti.

Kutokana na kunawiri kwa biashara ya 'bodaboda' katika kaunti, tunabuni mpango wa uchukuzi kwa biashara ya pikipiki hizo ambao utahusisha ujenzi wa vibanda vya bodaboda katika miji mikuu katika kaunti ndogo saba na baadaye kutoa mafunzo kwa waendeshaji bodaboda kuhusu utumiaji wa barabara na usalama.

Nimezindua ujenzi na kazi ya usawazishaji wa barabara ya Locher-Elim-Lorokon kama sehemu ya mpango wetu wa kustawisha maeneo ya mpakani. Mipango hii inalingana na juhudi zetu za kudumisha amani kuhakikisha kwamba kuna maendeleo ya muundo msingi kuambatana na juhudi za kutoa upya makao.

Mabibi na Mabwana,

Mnamo mwezi Aprili mwaka huu, tulisherehekea Tamasha za Utalii na Utamaduni (Tobong'u Lore) katika kituo cha kitamaduni cha Ekalees ambapo wageni wapatao 10000 walihudhuria, na kuchangia pakubwa uchumi wa eneo hili kwa kuzalisha mapato. Tamasha hizo pia ziliimarisha uhusiano baina ya jamii mbalimbali na maeneo tofauti kupitia kusherehekea utamaduni wetu wenye utajiri wa turathi.

Ili kuhamasisha kaunti yetu kupitia utalii, ujenzi wa Kituo cha Maonyesho ya Utalii/Kituo cha Habari za Utalii cha Lodwar umepiga hatua kubwa. Kandarasi imetolewa na kazi itaanza hivi karibuni fedha zitakapopatikana. Kitakapokamilika, hazina 50 za Kiutalii na habari muhimu kwenye Kaunti zitahifadhiwa kwa minajili ya wageni.

Idara ya Utalii inapanga kujenga maeneo ya biashara katika kaunti kulingana na aina ya biashara au shughuli inayopatikana mahala hapo kwa mfano, biashara ya mshubiri, Aloe Turkanensis, huko Lorengikipi, Lokichogio, Songot, Letea, Nawountos, Urum na Namoruputh, shughuli za gundi ya Arabic na utomvu huko Lorengippi, Loiya, Namoruputh, Lobei, Kalobeyei, Songot na Lokichar, Kilimomisitu na upanzi upya wa lishe ya mifugo huko Lobei, Kotaruk, Urum, Nawountos, Lokichoggio, Turkwel na Kerio. Asili ya mbegu za kuanzisha biashara zilizotajwa hapo juu ni kutoka Mlima wa Loima, misitu ya Turkwel, Kerio, Lapur na Kibish.

Serikali ya Kaunti imetoa mafunzo kwa wanawake 30 wanaotengeneza vifaa vya shanga mjini Lodwar na kuwapa maarifa ya utoaji na kuimarisha hali yao ya maisha kwa uuzaji wa vifaa vya sanaa. Hii ni sehemu ya mpango wa Ushanga Kenya ambao unanuia kuendeleaza na kusimamia utoaji wa vifaa vya shanga miongoni mwa wanawake wa Turkana.

Maonyesho ya Kitaifa ya vifaa vya sanaa vinavyotengenezwa kwa mikono yaliandaliwa katika kaunti ya Nairobi ambapo wanawake watatu walishiriki na kuonyesha vifaa vyao. Washiriki wakuu walipata maarifa ya uonyeshaji, uuzaji, uwekaji chapa na uwekaji bei.

Nikimaliza , ningependa kuchukua fursa hii kuwatakia watahiniwa wa darasa la nane na kidato cha nne ambao wanafanya mtihani wao mwaka huu, katika shule za umma na zile za kibinafsi, kila la kheri na ufanisi katika mtihani huo!

Nawatakia Mashujaa Dei yenye baraka!

Mungu abariki Kenya

Mungu abariki Kaunti ya Turkana,

Asanteni Sana!